**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA**

# T A N G A Z O LA NAFASI ZA KAZI

## 24/05/2022

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 chenye Kumb. Na FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapo chini.

**1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III-NAFASI KUMI NA MBILI (12)**

-

1.1 **Sifa za Mwombaji**

Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii,. kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.2. **Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III**

(i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
(ii) Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
(iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
(iv) Katibu wa Mikutano ya Kamati zote za Halmashuri ya Kijiji.
(v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
(vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
(vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika Kijiji.
(viii) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Vijiji

**1.3 Ngazi ya Mshahara**

Kwa mujibu wa ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS.B kwa mwezi

1.4 **Masharti ya ajira** - (Ajira ya kudumu)

2. **DEREVA DARAJA LA II - NAFASI NNE (4)**

**2.1. <u>Sifa za Mwombaji:</u>**

Kuajiriwa mwenye cheti cha Kidato cha nne (Form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

**2.2. <u>Majukumu ya Dereva Daraja la II</u>**

(i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari

(ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.

(iii) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.

(iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali

(v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.

(vi) Kufanya usafi wa gari, na

(vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

**2.3 <u>Ngazi ya Mshahara</u>**

Kwa mujibu wa ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS.B kwa mwezi

**2.4 <u>Masharti ya Ajira</u>**- (Ajira ya kudumu)

3. **KATIBU MAHSUSI III – NAFASI NNE (4)**

**3.1. <u>Sifa za Mwombaji:</u>**

Muombaji awe amehitimu kidato cha nne au sita na mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa ngazi ya tatu. Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta na kufaulu katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na awe amepata cheti katika programu za Microsoft Office Packages na Internent.

**3.2. <u>Majukumu ya Katibu Mahsusi Daraja la III</u>**

(i) Kuchapa taarifa, barua na nyaraka za kawaida

(ii) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu za kuhudumiwa

(iii) Kusaidia kutunza taarifa, kumbukumbu za matukio, miadi, wageni,tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba zingine zilizopangwa kutekelezwa katika katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA KILA MWOMBAJI**

(i) Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe na namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa(NIDA)
(ii) Muombaji awe na umri kati ya miaka 18-45
(iii) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jina au kufungwa jela.
(iv) Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji CV.
(v) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma,cheti cha kuzaliwa Nakala ya leseni kwa madereva na picha ndogo (Passport Size) ya hivi karibuni.
(vi) Testimonial, Result slip, Provisional Result, kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA**
(vii) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono
(viii) Waombaji waliosoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganifu na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.
(ix) Waombaji waliowahi kuacha kazi, kuachishwa kazi au kufukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama ana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi cha kuajiriwa upya.
(x) Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi yaani NTA levels maombi yatakayopokelewa na kufanyiwa kazi ni maombi ya cheti ngazi ya NTA Level 5 tu.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **06/06/2022** saa **9:30** Mchana

**Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-**

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga,
S.L.P. 22,
**Mahenge/Ulanga**
**MOROGORO.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
ULANGA

**SAIDA A. MAHUGU**
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
**H/W-ULANGA**

**Nakala:**

-Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320
DODOMA

-Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
www.ulangadc.go.tz

- Mbao za matangazo

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa